**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA JAMES FRANCIS MBATIA (MB) KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2016/17 NA MPANGO WA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017/2018**

*(Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9), toleo la mwaka 2016)*

## A: UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili niweze kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KRUB), kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 144 la terehe 22/04/2016 wizara hii imepewa majukumu makubwa ya kusimamia mambo yafuatayo: uandaaji wa sera za usanifu na ujenzi, usafiri na usafirishaji, tekinolojia ya mawasiliano, (ICT) Posta na simu na kusimamia utekelezaji wake, kusimamia ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko na maswala ya kiufundi, kusimamia kazi za umma na majengo ya umma, kusimamia shughuli za uhandisi na usanifu, usafirishaji wa reli na bandari; usafiri na usafirishwaji wa anga na viwanja vya ndege; utoaji wa leseni za usafirishaji, usalama katika usafirishaji na hali ya hewa; kuongeza tija

katika utendaji kazi pamoja na kuendeleza rasilimali watu na kusimamia Idara na taasisi zilizo chini ya wizara.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017.

### UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA ZILIZO CHINI YA WIZARA:

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano – Idara ya Ujenzi iliidhinishiwa shilingi 2, 176,204,557,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **1,831,365,922,000.00** ni fedha za ndani ambazo zilijumuisha fedha za mfuko mkuu wa serikali yaani consolidated fund shilingi 1,248,721,422,000 na fedha za mfuko wa barabatra shilingi 582,644,500,000.00. Aidha, shilingi **344,838,635,000.00** zilikuwa fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotolewa hadi machi, 2017 ni shilingi milioni 1,066,215.547 na kati ya fedha hizo shilingi milioni **853,422.431** ni fedha za ndani na shilingi milioni **212,793.11** ni fedha za nje. Ukiangalia takwimu hizo ni kwamba fedha za ndani zilizotolewa kwa kulinganisha na zile zilizopitishwa na Bunge ni asilimia **46.6** na fedha za nje zilizotolewa kwa kulinganisha na zilizokuwa zimeahidiwa ni asilimia **61.7.** Maana yake ni kwamba wahisani kwa ahadi zao wametekeleza zaidi kuliko upande wetu wakati miundombinu ni mali yetu.

**Mheshimiwa Spika**, fedha za maendeleo kwa idara ya mawasiliano zilitengwa shilingi 5,000,000,000.00 fedha za ndani na fedha za maendeleo kutoka nje 87,730,110,000.00. kiasi kilichotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka kwenye **fedha za ndani ni shilingi 190,309,000 sawa na 3.8%** huku fedha za nje zikitolewa shilingi 37,105,223,723.00 sawa na 40.2%.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inashindwa kuelewa ni kwa nini serikali inatoa fedha za maendeleo kutoka kwenye chanzo cha fedha zetu za ndani kwa 3.8% , huku tunawaaminisha watanzania kwamba tunatekeleza miradi ya maendeleo kwa fedha zetu za ndani, je tunadhamiria kuwadanganya watanzania au tunajidanganya sisi wenyewe?

**Mheshimiwa Spika**, hali haiko tofauti pia kwenye idara ya uchukuzi ambayo iliidhinishiwa shilingi **2,495,814,130,000.00** na kati ya fedha hizo shilingi 2,322, 603,400,00.00 ni fedha za ndani na shilingi 173,210,730,000 ni fedha za nje. Aidha hadi kufikia tarehe 31 Februari, 2017 kiasi cha fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi 761,494,685,101.99 sawa na 30.51% ya fedha zote za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha hizo zilizotolewa, kwa fedha za **ndani** za miradi ya maendeleo ni shilingi 816,995,812.07 ambazo ni sawa na **27.12%,** huku fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 131,677,689,289.92 ambazo ni sawa na 76.02% zilitolewa.

**Mheshimiwa Spika**, kambi rasmi ya upinzani bungeni inataka kupata ufafanuzi kuhusu fedha zinazotolewa na serikali, **yaani fedha za ndani**, kwanini kiasi kinachotolewa na serikali ni kidogo kulinganisha na fedha za nje zilizotolewa, kama tulivyoonesha hapo juu, je kuna tatizo gani ndani ya serikali kwenye jambo hilo na serikali ina utaratibu upi kuondoa tatizo hilo? Na ikiwa tunataka kweli kutekeleza miradi ya maendeleo kwa nini tusitoe fedha za ndani kwa asilimia kubwa kuliko fedha tunazotegemea kutoka nje?

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Wizara kukosa fedha za kutekeleza miradi ya mandeleo kama ilivyokuwa imekusudiwa ni dhahiri kwa mwaka huu wa fedha kumejitokeza matatizo ya kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali iliyoko chini ya wizara hii, kulimbikiza madeni ya wakandarasi wanaojenga barabara mbalimbali hapa nchini pamoja na miradi mingine ya kimaendeleo, ni kielelezo kwamba baadhi ya miradi ilishindwa kufanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inataka kupata majibu ya masuala yafuatayo:

i. Ni nini kilipelekea hazina kushindwa kutoa fedha kwa wakati kama zilivyokuwa zimepitishwa na Bunge na wakati huo huo serikali kupitia mamlaka ya mapato nchini (TRA) wakitoa taarifa ya kuongezeka kwa mapato. Ambapo hadi Machi 2017 TRA ilikusanya TSHS trilioni 10.87?

ii. Ni hasara gani imepatikana kwa serikali kutokana na ucheleweshwaji wa fedha hizo za maendeleo

iii. Kwa kuwa fedha nyingi zilizotengwa kwenye bajeti ya 2017/2018 zinakwenda kulipa madeni ya wakandarasi, je tutapaswa kuwalipa riba au tozo la ucheleweshaji malipo kiasi gani baada ya serikali kushindwa kutekeleza mkataba wa malipo kwa wakati.

**Mheshimiwa spika**, kwa Mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, toleo la 2005, Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano **chenye madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri serikali** ya Jamhuri ya Muuungano na **vyombo vyake vyote** katika **utekelezaji wa majukumu** yake kikatiba.

**Mheshimiwa spika**, katika muktadha huo, ikiwa serikali inakusanya mapato hadi kuvuka lengo lake la ukusanyaji na ikiwa Taifa lilijiwekea Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano ambao uliidhinishwa na Bunge lako tukufu, na ikiwa Serikali pamoja na kukusanya mapato kupita lengo la ukusanyaji waliojiwekea lakini bado, fedha kwa miradi ya maendeleo hazipelekwi hata nusu, kwa mujibu wa takwimu za Wizara hadi mwezi February 2017.

**Mheshimiwa spika** tunapaswa kujiuliza wapi kuna tatizo, hata kama Serikali ya Chama Cha Mapinduzi haipendi kukiri kuhusu hali hii mbaya lakini bunge hili tunao wajibu kwa mujibu wa ibara ya 63 ya katiba, kuisimamia serikali.Aidha viashiria vya kupeleka fedha kidogo kwenye

miradi ya maendeleo wakati Serikali inakusanya fedha zaidi ya malengo iliyojiwekea ni ishara kwamba kuna tatizo la msingi sehemu ambayo serikali haitaki kuliweka wazi.

## C. BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/ 2018

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ujenzi fungu 98 imetengewa jumla ya shilingi **2,176,204,557,000/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni ya kimkakati na isiyo ya kimkakati. Na kati ya fedha hizo shilingi **1,831,365,922,000/-** ni fedha za ndani na zilizobaki ni kutoka nje. Aidha sekta ya ujenzi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imetengewa jumla ya shilingi 1,932,850,115,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo , shilingi 1,350,000,000.00 ni fedha za ndani kutoka mfuko mkuu wa serikali na shilingi 582,850,115,000.00 ni fedha za nje na shilingi 682,284,000,000.00 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya mfuko wa barabara.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha ni pungufu kwa shilingi 243,354,442,000.00 ukilinganisha na makadirio ya mpango wa bajeti ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mwaka 2016/2017. .Aidha vipaumbele vya miradi vitakavyotekelezwa ni miradi inayoendelea kutekelezwa, miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na miradi iliyopo kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka Mitano,uliowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwaka jana na mpango

ambao kwa mujibu wa Wizara hii, hauendani na miradi iliyowasilishwa kwenye bajeti ya wizara hii. Aidha baadhi ya miradi ambayo iko kwa mujibu wa mpango wa maendeleo ya miaka miatano, ambayo ilipaswa kutekelezwa, miradi mingine haipo na miradi mingine imetengewa kiasi kidogo kinyume na mpango uliopitishwa na Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano(2016/17-2020/21), mradi wa Dar es salaam- Chalinze- Morogoro Express way, (200-km)kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 unapaswa kutengewa (Tshs. Billion) 231.16 lakini kwenye randama mradi huo unaonekana ukitengewa kiasi cha Million 12,771.00. Mradi wa Ujenzi wa fly over eneo la TAZARA, mradi ambao kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, mradi huu ulipaswa kutengewa 53.27 billion lakini mradi huu umetengewa shilingi Millioni 25,564.000. Ujenzi wa mradi wa njia ya mchepuko (construction of interchange at Ubungo) mpango wa miaka mitano unataka mradi huu kutengewa 74.23 (Tshs Billion) lakini kwenye randama kiasi kilichotengwa ni 20,326.000 (shilingi milioni)

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano hapo juu, maana yake ni kwamba miradi itakayotekelezwa ni ile inayoendelea sasa, ambayo kimsingi mingine ilikwama kutokana na serikali kutopeleka fedha kwenye miradi hiyo, Miradi inayofadhiliwa na washirika wa Maendeleo na miradi hii iliyoko kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambayo

nimeionesha hapo juu kwamba haijapangiwa fedha kama mpango wetu unavyotuelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kuwa makini na kutekeleza vipaumbele kama ambavyo vimepangwa. Kwa kutotekeleza mpango wa Taifa , maana yake ni kwamba Bunge lako tukufu lilitumia rasilimali fedha na muda kama kivuli tu, huku serikali ikifahamu kuwa mpango huo hautekelezeki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ipo haja ya kudurusu mpango huo kama unatekelezeka pia kuna haja ya kuwepo kwa sheria mahususi ya kusimamia mpango.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali katika Bajeti iliyopita ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **58,004,000.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato ambazo ni idara ya utawala, idara ya huduma za ufundi na idara ya menejimenti ya ununuzi na ugavi.

Na kwa kuwa serikali kupitia taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano imekiri kwamba hadi kufikia mwezi februari, 2017 Serikali imefanikiwa kukusanya shilingi 28,290,000.00 sawa na 48.77% ya malengo ya mwaka wa fedha 2016/2017,

NA KWA KUWA Serikali katika makadirio ya mpango na bajeti ya wizara ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi **62,002,000.00** kutoka idara ya tawala na

rasilimali watu, idara ya huduma za ufundi na idara ya na idara ya menejimenti ya ununuzi na ugavi.

NA KWA KUWA, kiasi cha fedha kinachotazamiwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, cha shilingi 62,002,000.00 ni kikubwa kuliko makadirio ya mwaka 2016/2017 ambapo shilingi 58,004,000.00 zilitarajiwa kukusanywa na hivyo kufanya makadirio ya makusanyo kwa mwaka huu wa fedha kuongezeka kwa shilingi 3,998,000.00

NA KWA KUWA vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni vile vile vilivyoainishwa kutumika mwaka wa fedha 2017/2018

**Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani** bungeni inaitaka serikali kulieleza bunge hili tukufu;

i. Mosi, sababu zilizopelekea wizara hii kushindwa kukusanya mapato yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zaidi ya nusu ya matarajio ya makusanyo waliyojipangia kukusanya kutoka vyanzo hivyo hivyo vinavyoorodheshwa sasa.

ii. Pili, Serikali iliambie bunge lako tukufu mikakati thabiti na endelevu ambayo wizara hii imakuja nayo ili kuhakikisha makadirio ya makusanyo yanaongezeka badala ya utaratibu wa sasa wa kuongeza idadi ya fedha tu, kwa mikakati ile ile, na vyanzo vya mapato bila ubunifu wowote unaoongezeka, ikizingatiwa kwamba vyanzo vya mapato vya idara ya utawala na rasilimali watu, idara ya huduma

za ufundi na idara ya menejimenti ya ununuzi na ugavi vyote kwa pamoja vilishindwa kukusanya hata nusu ya makadirio kwa mwaka 2016/2017.

iii. Tatu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa ufafanuzi wa sababu ya utaratibu wa kuongeza takwimu kwenye bajeti, huku ikijua kabisa kwamba hakuna uhalisia wowote baina ya namba kubwa za takwimu zinazoongezwa na au kutajwa na uhalisia wa makusanyo ya mapato, je kufanya hivyo kuna maana nyingine zaidi ya kuwa hadaa watanzaniana wananchi kwa ujumla?

**Mheshimiwa Spika,** kushindwa kutekelezwa kwa miradi hiyo ya maendeleo kama ambavyo serikali iliwaahidi watanzania, kupitia bajeti yake ya 2016/2017 ni dalili tosha kwamba mabadiliko ambayo watanzania waliahidiwa kupitia bajeti hiyo, yalikuwa matumaini hewa na hivyo jamii ya Kitanzania sasa inazidi kushuhudia matatizo yanayotokana na miundombinu mibovu yakishindwa kukamilika kutokana na bajeti ya serikali kushindwa kutekelezeka hata kwa kiwango cha asilimia 50%. Ucheleweshaji wa kumalizika miradi ya ujenzi pamoja na ongezeko la gharama za miradi ambazo kwa kiasi kikubwa hutokana na uwepo wa masilahi binafsi ya wachache katika nchi yetu vimezidi kuwa changamoto katika awamu hii ya tano ya serikali hii.

**Mheshimiwa Spika,** wakati akiwasilisha maoni ya kambi Rasmi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, alisema mbele ya bunge lako tukufu kuwa barabara za lami zilizojengwa

tangu tupate uhuru mwaka 1961 kwa kiwango cha lami ni wastani wa asilimia 16 tu ya barabara zote nchini zenye urefu wa zaidi ya kilometa 35,000. Kwa kasi hiyo ya ujenzi ingeligharimu Taifa zaidi ya miaka 62 ijayo ili kukamilisha ujenzi wa kilometa 29,432 ambao ni sawa na asilimia 84 ya barabara zote zilizosalia kujengwa kwa kiwango cha lami nchini bila kujumulisha barabara mpya zinazosanifiwa mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya upinzani Bungeni pia ilinukuu sehemu ya hotuba ya aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi ambaye kwa sasa ni Rais wa serikali ya awamu ya tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliyowasilisha katika bunge la 10, na kukiri kuwa Serikali ya CCM katika awamu ya nne ilishindwa kutekeleza ilani zao kikamilifu za uchaguzi za mwaka 2005 mpaka mwaka 2015, kwa kujenga barabara nchini kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 5,568 sawa na asilimia 31 kwa lengo walilojiwekea la kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 17,762.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya hotuba hiyo, ambayo pia ili nukuliwa na Kambi Rasmi ya uUpinzani Bungeni ilisema;

> *"**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha serikali ya awamu ya nne, serikali imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja nchini. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 17,762 zimekuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 5,568 zimekamilika*

*kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 3,873 zimeendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa 4,965 zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na serikali inatafuta fedha za kuzijenga kwa kiwango cha lami. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye jumla ya kilometa 3,356 unaendelea"*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka Serikali hii ya awamu ya tano, kutoa maelezo ya kina mbele ya bunge hili kuhusu mipango ya uhakika na endelevu ya kukamilisha ujenzi wa barabara hizo kwa viwango vinavyokubalika kimataifa na kwa kuzingatia vipaumbele kwa misingi ya kitaalamu, badala ya ahadi nyingi zisizotekelezeka.

**Mheshimiwa spika**, Pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuitaka serikali kufanya hivyo, na pamoja na ukweli kwamba aliyekuwa waziri wa ujenzi katika kipindi cha serikali ya awamu ya nne, ndiye Raisi wa jamhuri ya muungano wa Tanzania lakini bado utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika wizara ya ujenzi, mawasiliano na uchukuzi umezidi kudorora na hali hii inaudhihirishia umma wa watanzania walio wengi kwamba hakuna utofauti wowote wa kimipango na mikakati thabiti ya kutatua tatizo la barabara hapa nchini kwa kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo inatekelezwa chini ya 50%

## D. SEKTA YA UJENZI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kupitia Wizara hii imeendelea kushindwa kutekeleza kikamilifu ahadi zake ilizozitoa mara kwa mara za kujenga barabara kwa viwango bora pamoja na vivuko, badala yake jamii ya kitanzania imeendelea kukumbana na changamoto za usafiri, mijini na vijijini. Katika jiji la Dar na majiji mengine yanayokua kwa kasi kama vile Mbeya,Mwanza, Arusha na muda si mrefu Dodoma msongamano wa magari barabarani hasa vipindi vya asubuhi na jioni limeendelea kuwa kero kwa wananchi wengi, hivyo kuchangia nguvu kazi kutokutoa tija inayokusudiwa..

**Mheshimiwa Spika**, katika maeneo ya vijijini hususan vipindi vya mvua, barabara nyingi nchini huwa hazipitki na TANROADS na Halmashauri za Wilaya kushindwa kutoa huduma za matengenezo. Hali hii imekithiri katika mikoa yenye mvua nyingi kama vile; Njombe, Iringa, Mbeya, Morogoro.

**Mheshimiwa Spika**, maandiko yanasema kuwa Tanzania inaelekea kuwa nchi ya uchumi wa viwanda ambao kwa sehemu kubwa itategemea mazao ya wakulima kufika sokoni kwa muda unaohitajika. Jambo hili litaendelea kuwa nadharia kama serikali hawatakuwa na mipango makini yenye vipaumbele vinavyotekelezeka.

**Mheshimiwa Spika**, maneno upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, matangazo ya tenda yamekuwa ni kichaka cha kujifichia kwa serikali hii ya CCM.  Kambi Rasmi ya Upinzani

haipingani na hatua hii ya kihandisi, lakini mara nyingi hatua hizi zimetumia fedha nyingi na matunda yake hayaonekani. Hivyo tunaitaka Serikali kuweka muda maalum wa kumaliza hizo ngonjera ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili miradi ijulikane ni lini miradi inaanza na kumalizika.

**Mheshimiwa Spika,** Nchi hii tunayo sera inayotoa kipaumbele kwa kujenga kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha mikoa yetu. Pamoja na uwepo wa sera hii ni muda sasa bado mikoa mingi haijaunganishwa kama vile Arusha- Mara, Arusha-Simiyu, Manyara –Simiyu, Manyara-Tanga, Morogoro –Ruvuma, Morogoro –Lindi, Mbeya-Njombe n.k

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza watanzani ni lini barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami kama sera inavyosema.

1. **KUPANDISHWA HADHI/ KUKASIMISHWA BARABARA ZA WILAYA KUWA BARABARA ZA MKOA/ TANROADS**

**Mheshimiwa Spika**, Halimashauri nyingi nchini kama si zote zimekuwa zikipeleka wizarani maombi ya kupandisha/ kukasimu barabara hizo kuwa barabara za mkoa, kwa wakala wa barabara (TANROADS) baada ya barabara hizo kukidhi vigezo na baada ya maombi hayo kupitia vikao halali ngazi za wilaya na mikoa

**Mheshimiwa Spika,** matengenezo ya barabara yanahitaji fedha nyingi na kwa vile serikali kuu haipeleki fedha za kutosha kwa halimashauri, uwezo wa kuzishughulikia

unakuwa ni mdogo mno. Aidha ni muda mrefu umepita tangia barabarani zipandishwe hadhi. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuu kupitia TANROADS ione haja ya kuzipandisha barabara mara kwa mara ili kutoa unafuu wa matengenezo kwa halimashauri lakini pia kuzijenga kwa ubora zaidi.

## II. MADENI YA MAKANDARASI NA WAHANDISI WASHAURI WA MIRADI YA BARABARA.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari 2017, makandarasi na wahandisi washauri walikuwa wanaidai serikali takribani shilling billioni 788 ikilinganishwa na deni lililokuwepo 30/06/2016 la takribuni shilingi bilioni 930.

**Mheshimiwa Spika,** huu siyo utaratibu mzuri kwa serikali kuendelea kuwakopa makandarasi ili hali wameshamaliza au kukamilisha wajibu wao wa kimkataba na kwa wale ambao hawajakamilisha ujenzi wa miradi yao huongeza kasi ya utekelezaji kutokana na namna ambavyo serikali imekuwa ikitoa fedha kwao. Kwa maana nyingine mheshimiwa spika, kutowalipa wakandarasi kwa muda unaotakiwa na kadri ya mikataba imekuwa na athari kubwa ikiwemo miradi kutokamilika kwa muda na pia kuongezeka kwa gharama zinazotokana na riba. Ikiwa serikali ya awamu ya tano imekuwa ikijigamba sana kwamba inakusanya fedha nyingi na majigambo hayo ni ya kweli, Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaitaka serikali

kulipa madeni yote ya makandarasi na wahandisi washauri. Kuna msemo unaosema “ujanja ni kulipa na siyo kukopa”

### III. UTAWALA WA SHERIA NA MIRADI INAYOJENGWA:

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu dhamira ya serikali kuhusu miradi mbalimbali inayoendelea kujengwa hapa nchini; pamoja na dhamira hii kuna tatizo la kutofuatwa kwa sheria za nchi zinazohusu utoaji wa tenda na manunuzi ya umma. Katika siku za mwanzo wa utawala wa awamu ya Tano, Serikali ilisitisha shughuli za sherehe za uhuru na kuamriwa pesa ambazo zingetumika kwenye sherehe hiyo zielekezwe kwenye upanuzi wa barabara ya MWENGE, Tunafahamu pia umuhimu na dhamira ya kujenga mabweni ya chuo kikuu cha Dar es salaam pamoja na ujenzi wa nyumba za kota eneo la Magomeni.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema lakini si busara kukiuka sheria na kanuni tulizojiwekea ili kuendesha sekta hii ya ujenzi. Swali tunalojiuliza na ambalo watanzania wengi wanataka kupata ufafanuzi ni je, serikali ilitangaza lini tenda za miradi yote mitatu iliyotajwa hapo juu, kama ndiyo tenda hizo zilitangazwa kwa kipindi gani na nani aliyeshinda tenda hizo? Ikiwa hakuna utaratibu wa kutangaza tenda hizo ni kwanini serikali yenye jukumu la kuilinda na kuitetea katiba ya nchi pamoja na sheria zake inakuwa ya kwanza kutofuata sheria hizo huku ikiwataka wananchi watii sheria bila shuruti?

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 13, machi 1995 Baba wa Taifa Mwalimu Julius K.Nyerere aliongea na watanzania kupitia hotupa yake kwa klabu ya waandishi wa habari wa Tanzania. Katika hotuba hiyo Hayati Mwalimu Nyerere alilieleza taifa kuwepo kwa nyufa katika taifa letu, na miongoni mwa nyufa hizo ilikuwa ni pamoja na ufa wa pili aliouita "kupuuza na kutokujali katiba, pamoja na ufa wa tatu aliouita kuendesha mambo bila kujali sheria

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Mkuu wa nchi kutoa kibali cha ujenzi kwa baadhi ya wakandarasi bila kufuata taratibu za kutoa tenda kinaacha maswali mengi ya kujiuliza hata kama mheshimiwa Rais alikuwa na nia njema, lakini sasa wananchi lazima wajiulize kuhusu serikali yao, kuna maslahi gani na wakandarasi waliopewa majukumu ya kukamilisha ujenzi wa miradi hiyo? Je umuhimu wa kuwa na sheria pamoja na taratibu za kusimamia tenda za serikali umesitishwa au hautumiki tena?

## E. SEKTA YA UCHUKUZI

## I. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE (TAA)

**Mheshimiwa spika** mamlaka ya viwanja vya ndege nchini (TAA) ndiye mmliki wa viwanja vya ndege hapa nchini, kati ya viwanja vyote hivyo, ni viwanja 2 tu, ambavyo ni viwanja vya Kilimanjaro, na Dar es salaam ndivyo vyenye uwezo wa kujiendesha. Viwanja vilivyobaki havina uwezo wa kujiendesha kutokana na mapato duni yanayozalishwa kutokana na viwanja hivyo, hivyo gharama za uendeshaji

hutegemea mapato yanayopatikana kutoka katika viwanja vitatu tu.

**Mheshimiwa spika**, kwa hali hii ni dhahiri kabisa kwamba sekta ya usafiri wa Anga nchini inakabiliwa na changamoto kubwa ambazo ni pamoja na miundombinu hafifu, matatizo ya menemejimenti, kushindwa kutolewa kwa fedha za kukamilisha miradi ya viwanja vya ndege kama ambavyo imeidhinishwa na Bunge hili tukufu.

## II. UWANJA WA NDEGE WA MWALIMU JULIUS NYERERE (TERMINAL THREE)

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa jengo la tatu la abiria (terminal III) katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulitengewa bilioni 26, Aidha fedha hizi hadi kufikia mwezi December 2016 zilikuwa hazijatolewa.

**Kambi Rasmi ya Upinzani** inaitaka serikali kutoa ufafanunuzi, ni kwanini fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi kama hii muhimu zinakuwa hazitolewi?

## III. UJENZI WA UWANJA WA NDEGE WA SONGWE:

**Mheshimiwa Spika**, Uwanja wa ndege wa Songwe ni kiungo muhimu, katika sekta ya uchukuzi hasa ukizingatia maeneo yanayohudumiwa na uwanja huo. Kwa takribani miaka miwili mfululizo ujenzi wa uwanja huu umekuwa ukisua sua bila serikali kutoa sababu za msingi, wakati kuna viwanja

vimeanza kujengwa hivi karibuni hapa nchini na maendeleo yake yanaonekana kila kukicha. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 5. Mwaka wa fedha uliofuata 2016/2017 mradi huu pia ulitengewa fedha shilingi bilioni 7 lakini pia kufikia mwezi December 2016 hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya mradi huu.

Ikiwa mradi huu unahitaji kiasi cha shilingi bilioni 16.154 ili kukamilisha ujenzi wake, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni, kuwa serikali wakati inafanya majumuisho hapa watoe kauli kwa wananchi wanao tarajia huduma bora kutokana na uwanja wa ndege wa Songwe, kuhusu sababu za msingi za kutopewa kipaumbele wakati huo huo miradi mingine ikipewa kipaumbele kutekelezwa.

## IV. MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)

### BANDARI YA DAR ES SALAAM

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imebahatika kuwa na ukanda mrefu wa bahari na pia kuwa nchi inayoweza kuhudumia mataifa ambayo Kijiografia hazijapakana na Bahari na hivyo kuwa kitovu cha biashara katika ukanda huu kama ilivyo Dubai, Singapore na Hongkong kwani imepakana na nchi sita zisizokuwa na Bandari.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na bahati hii ya kijiografia, bado bandari zetu, Reli zetu zimeshindwa kutoa ushindani wa kibiashara kwa bandari zingine za ukanda huu. Bandari

ya Dar es Salaam ambayo hapa kwetu ndiyo kubwa kuliko zote, imeendelea kuwa ya mwisho ikilinganishwa na bandari za ukanda huu kama vile Durban, Beira na Mombasa.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto nyingi katika bandari yetu ambazo zimeongelewa mara ni nyingi ni pamoja na zifuatazo; lango dogo kuweza kupokea meli kubwa, kinakifupi cha maji, Kodi ya VAT on auxillary goods, ushuru wa himaya moja ya forodha (SCT), urasimu uliokithiri n.k hivyo vyote vimechangia kupoteza wateja, shehena ya mizigo na pia mapato ya Serikali kuendelea kushuka kila kukicha.

## V. UJENZI WA GHATI NAMBA 13 & 14 BANDARI YA DAR ES SALAAM

**Mheshimiwa spika**, Hotuba ya msemaji mkuu wa kambi rasmi ya upinzani bungeni kwa wizara hii, katika mwaka wa fedha 2013/2014, kipengele cha 3.3.1 kuhusu ujenzi wa ghati 13 & 14 bandari ya Dar es salam ilisema na ninaomba kunukuu kwa lengo la kuikumbusha serikali

> **"*Mheshimiwa spika***, *kutokana na kandarasi iliyotolewa na mamlaka ya usimamizi wa Bandari kwa kampuni ya China Communication Construction Ltd iliyoleta mtafaruku mkubwa hapa nchini wa kujenga ghati namba 13&14 katika bandari ya Dar es salaam, mpango ambao ulitokana na mpango mkuu wa bandari (Port Master Plan 2009-2028) mradi ambao ulikisiwa kutumia kiasi cha Dola za kimarekani milion 323*

*sawa na bilioni 517 fedha za kitanzania"* kwa kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi kuhusu uteuzi wa mshauri muelekezi na mkandarasi katika mradi huu iliyotolewa tarehe 9 Novemba 2012 na PPRA kamati ya uchunguzi kuhusu uteuzi wa mshauri muelekezi na mkandarasi wa ujenzi wa Ghati namba 13 & 14 katika Bandari ya Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa katika Bunge la 10 mkutano wa saba wa Bunge hilo kulikuwa na majadiliano ya kina kuhusiana na ujenzi wa ghati hizi, na Bunge liliagiza kuwa mradi huu utekelezwe kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya China kama ilivyopendekezwa na Mamlaka ya Bandari.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka kupata majibu juu ya masuala yafuatayo:

a. Mchakato wa ujenzi wa Ghati 13 & 14 umefikia wapi mpaka sasa?

b. Baada ya kusitishwa kwa mchakato na mkataba wa awali ni hatua gani zimechukuliwa na serikali dhidi ya waliohusika na mchakato ambao ulikiuka sheria za nchi.

c. Ni lini ujenzi wa Ghati hizi utakamilika ili kuweza kuendana na mpango mkuu wa bandari nchini?

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kufanya hivyo, serikali haikuona nia thabiti ya kutekeleza mradi huo. Aidha miaka miatatu baadaye kamati ya bunge lako tukufu nayo inaona kuna tija kwa serikali kujenga gati namba 13 & 14 kama mkakati wa kuliongezea taifa mapato. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inasisitiza ushauri huo kama ilivyoshauri katika bajeti ya mwaka 2013/2014, ushauri ambao sasa kamati ya bunge ya miundombinu pia imeendelea kushauri katika vikao vyao na TPA.

## VI. USAFIRISHAJI MAJINI:

### a. KIVUKO CHA MV DAR ES SALAAM

**Mheshimiwa Spika**, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni katika mwaka wa fedha 2016/2017 alihoji kuhusu kivuko hiki, baada ya ripoti ya mkaguzi na mthibiti wa hesabu za serikali kubainisha kwamba kivuko hicho hakikuwa na "delivery certificate" pamoja na madhaifu mengine ya kivuko hicho kutotimiza matakwa ya kimkataba.

Aidha Serikali ilikiri mbele ya Bunge lako Tukufu na kwa mujibu wa Hansard, serikali ililiambia Bunge hili kwamba Kivuko kile hakikupokelewa kwa sababu hakikuwa na vigezo vya kimkataba na kwamba badala yake, kampuni iliyoiuzia Tanzania kivuko kile ilikuwa inakifanyia matengenezo ili kiweze kukidhi vigezo vya kimkataba

likiwemo tatizo la speed ambalo lilikuwa kinyume na matakwa ya kimkataba.

**Mheshimiwa Spika**, wakati ambapo watanzania wanasubiri taarifa ya kama ukarabati wa kivuko kile umekamilika na kama kivuko kile sasa rasmi kimekadhiwa kwa serikali, Serikali kupitia Mheshimiwa Rais mapema mwaka huu aliutangazia umma wa Tanzania kwamba kivuko hicho sasa ni mali ya jeshi la wananchi wa Tanzania. Taarifa hiyo aliitoa katika hotuba fupi baada ya sherehe fupi za kuapishwa kwa ***wateule wake katika jeshi,polisi na mashauriano ya kigeni,*** Mheshimiwa Rais Magufuli alinukuliwa akisema ile meli/kivuko cha "Mv Dar es Salaam" ambacho watu wamelikuwa wakiisemasema, sasa nimeamua kukigawa kwa JWTZ kikosi cha Wanamaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni haioni tatizo la maamuzi hayo ya Mheshimwa Rais ikiwa lengo la kugawa Kivuko hicho ni kurahisisha ulinzi na patrol katika eneo la bahari ya Hindi ili kuweza kudhibiti magendo na uingizaji wa bidhaa haramu pamoja na wahamiaji haramu wanaotumia pwani na fukwe za bahari ya Hindi kuingia ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na nia hiyo thabiti tunayokubaliana nayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu mambo yafuatayo:

i. Ni lini marekebisho ya kivuko hicho yalikamilika, na ni lini kivuko hicho kilikabidhiwa kwa serikali Rasmi kwa maana ya kupokea Derivery certificate?

ii. Kwa vile bajeti ya kununuliwa kwa kivuko ililenga kuondoa tatizo la usafiri kutoka Dar es salaam hadi Bagamoyo mkoani Pwani, na sasa kivuko hicho kimebadilishwa matumizi na kukabidhiwa kwa Jeshi letu, Je, serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kununua kivuko kingine ambacho kitafanya kazi ambayo ilikusudiwa kufanywa na kivuko cha MV-DAR ES SALAAM?

iii. Kutokana na malengo ambayo umma wa watanzania tuliambiwa kwamba kivuko kinakwenda kufanya , je kivuko kile ambacho kilisanifiwa na kutengenezwa kwa ajili ya kusafirisha abiria, kinakithi vigezo kwa matumizi ya kijeshi kama ilivyotangazwa?

### b. USAFIRI KATIKA ZIWA VICTORIA

**Mheshimiwa Spika,** usafiri katika ziwa Victoria kwa wananchi wa mikoa na wilaya zinazolizunguka ziwa hili imekuwa ni changamoto kwa kiasi kikubwa. Katika ziwa hili meli mbili za serikali zilizokuwa zinatoa huduma ya usafiri kwenda kisiwa cha Ukerewe (Mv Butiama na Mv Clarius) zote ni mbovu kwa kipindi kirefu sasa na hivyo wananchi kutegemea usafiri wa meli binafsi ya Mv Nyahunge ambao haukidhi mahitaji na kusababisha adha kubwa ya usafiri.

Katika bajeti ya 2016/2017 serikali ilitenga jumla ya shilingi Tsh 3.5 billion kwa ajili ya meli ya Mv Butiama lakini hadi sasa hivi matengenezo bado hayajaanza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka serikali kutoa kauli ya lini fedha

hizo ambazo ziliidhinishwa na bunge lako tukufu zitatolewa ili wananchi wa ukerewe waondokane na kero ya usafiri.

**Mheshimiwa Spika,** Meli ya Mv Clarius ni meli iliyochoka na kuchakaa sana kwani imekuwepo tangia enzi ya mkoloni, jukumu la kutengeneza meli hii wameachiwa Marine Service Company Ltd (MSCL) ambao nao wamechoka sana maana hata kulipana mishahara yao ni shida hadi kulipwa na Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inajiuliza kampuni hii inapataje uwezo wa kutengeneza meli? Aidha ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuitaka serikali kuja na suluhisho la usafiri wa uhakika kisiwani Ukerewe. Hasa ukizingatia kuwa mzabuni aliyeshinda hatua ya awali ya ununuzi wa meli moja ameshindwa kukidhi matakwa ya zabuni baada ya kuleta taarifa za ufundi.

## VII. UJENZI WA RELI YA KATI NA MATAWI YAKE

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa reli hii umegawanyika katika vipande vinne vya Dar es salaam – Morogoro (km 202), morogoro – Makutopola (km 336), makutopala – Tabora ( km 294), Tabora – Isaka (km 133) na Isaka – Mwanza (km 254). Aidha mkataba tulio nao na kampuni ya kutoka nchini UTURUKI ni wa kujenga kipande cha Dar es salaam – Morogoro. Bado ujenzi wa vipande vingine vya reli haviko katika mpango wowote na kwa kuwa ujenzi wa reli hii pia ni ushindani wa mizigo iliyoko nchini Jamhuri ya Kidemkrasia ya Kongo, (DRC) Burundi na Rwanda na kwa kuwa tunafahamu pia kwamba nchi washindani wanajenga reli

kama hii kutoka Mombasa- Uganda- Rwanda ambako ujenzi wake uko katika hatua za mbele zaidi.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** ina wasiwasi mkubwa, nikirejea kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba ili mradi huu uwe **“economically viable”** ni lazima tuweze kupata mizigo kutoka nchini DRC na Burundi. Hivyo ujenzi wa vipande vifupi vifupi na kuacha eneo ambalo litaweza kuleta faida kiuchumi kama ushauri wa Waziri wa fedha ulivyokuwa, inaonekana ni hasara kubwa kwa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Umesainiwa mkataba wa Tsh trilioni 2.5 ujenzi wa reli ya Dar es salaam – Morogoro zote zikiwa ni fedha za ndani kama Mhe Rais alivyosema, lakini pale pale anasema Waturuki ndio watajenga kwa fedha za mkopo, Kambi Rasmi inataka kufahamu ukweli ni upi katika hilo?

**Mheshimiwa Spika**, awali Watanzania tuliaminishwa kuwa Reli hii mpya itajengwa na Wachina kwa kutumia mkopo toka EXIM Bank ya Uchina. Tanzania ilituma timu ya viongozi Uchina akiwemo Rais Mstaafu wa Awamu ya NNE, Waziri wa Ujenzi na timu hiyo iliporudi tuliambiwa China imekubali kutusaidia na  hatajenga kipande hiki cha Dar-Moro, ilipotangazwa makampuni mengi ya Kichina yalichukua vitabu lakini hawakuvirudisha.

**Mheshimiwa Spika**, hivi sasa Reli inajengwa na Kampuni ya Kituruki kwa mkopo na mkataba wa miezi 30

kukamilisha. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze watanzania ni nini kimetokea kwa mkopo uliokwisha kubalika toka Uchina?

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zilizochapishwa na gazeti la kila siku la The Citizen katika ukurasa wa mbele zilieleza kuwa benki ya Exim kutoka china ilikubali kutoa mkopo wenye riba nafuu wa Tsh trilion 17.5 au dola za Kimarekani bilioni 7.6 kwa ajili ya kuanza rasmi na kukamilisha ujenzi huo wa reli ya kati huku serikali ya Tanzania ikitangaza kutoa Tsh trilion 1, kwa ajili ya hatua za awali za mradi huo. Aidha baadhi ya watanzania pia wanafahamu kuwa Tanzania iliomba mkopo wa fedha kutoka India kiasi cha Tsh Trilion 17.5 ili kufanikisha ujenzi wa reli ya kati.

**Mheshimiwa Spika,** habari ya Benki ya Exim ya China kukubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu wa dola za Marekani Bilioni 7.6 sawa na Zaidi ya shilingi trilion 17.6 za kitanzania kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa mradi mkubwa wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa, na taarifa za utiaji saini makubaliano ya awali ya ujenzi wa reli ya kati (standard gauge) ziliripotiwa pia na serikali kupitia kitengo cha mawasiliano Serikalini,Wizara ya Ujenzi , Uchukuzi na Mawasiliano na shirika la Utangazaji la Uingereza BBC, tarehe 20 julai , 2016 . Aidha kwa mujibu wa taarifa hiyo, mradi wa ujenzi wa reli ya kati utahusisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha kisasa kutoka Dar es salaam – Tabora- Isaka- Mwanza. Tabora – Mpanda –

Kalemela. Tabora – Uvinza- Kigoma na Isaka- Keza – Msongati.

**Mheshimiwa spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka serikali kutoa kauli sahihi kuhusu mkanganyiko huu, je, Ni kweli reli ya kati inajengwa kwa fedha za ndani kama ambavyo inasemekana? Ikiwa ni ndiyo je mkopo kutoka benki ya Exim China unahusu ujenzi wa reli ipi na nini kilichotokea makampuni ya China ambayo yalikuwa awali yanatajiwa kujenga mradi huu kutojenga na ghafla kampuni ya kutoka nchini UTURUKI ikapewa tenda hiyo? Ni vyema watanzania ambao wanawajibika kulipa mikopo hii kupitia kodi zao, wakaondolewa sintofahamu iliyopo miongoni mwao.

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Rais wakati akizindua ujenzi wa reli ya kati alinukuliwa akiwaambia watanzania kuwa dereva mzuri wa lori ni yule ambaye hasikilizi kelele za abiria wake na yeye kama Dereva hatasikiliza kelele hizo. Kelele hizo yamkini ni maoni yanayotolewa dhidi ya miradi mbalimbali inayoendelea hapa nchi; Aidha kauli hiyo pia inakiuka ibara ya 63 ya katiba ya nchi, kwa kuwa kuishauri serikali siyo kupiga kelele kama inavyodaiwa. Pamoja na hayo haijalishi kama kelele hizo zina nia njema au hazina nia njema, anachosema dereva huyu ni kwamba hayuko tayari kusikiliza ushauri wowote, uwe mzuri au mbaya anachoamini ni kwamba yeye anafahamu kila kitu na hapaswi kushauriwa. Aidha pamoja na kasumba hii ya serikali hii ya awamu ya tano,

ya kutopenda kupokea ushauri hata ukiwa na tija kiasi gani kwa taifa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kurudia ushauri ufuatao kwa manufaa ya taifa letu la Tanzania kuhusu ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa;

i. Taifa linahitaji reli inayojengwa, kujengwa kwa mtazamo mpya wa kisasa na wa upeo wa miaka mingi ijayo. Tunahitaji reli ambayo itaendana na mazingira tuliyonayo ya ukubwa wa nchi na fursa tuliyonayo ya nchi zilizotuzunguka zinazotegemea bandari zetu. Aidha hoja za mwendo kasi na uwezo wa kubeba uzito mkubwa ni vitu vya kuzingatia katika ujenzi huo.

ii. tunashauri na tunaendelea kushauri reli ijengwe kwa mtazamo wa mbali wa zaidi ya miaka 50 ijayo, tuanze na reli moja sambamba na hii iliyopo, lakini mpango uwe kuwa na zaidi ya reli moja hapo baadaye ili kuwezesha usafirishaji katikati ya Tanzania na nchi jirani kuwa wa muda mfupi zaidi, ili kuzivuta nchi jirani kuona reli yetu ndiyo ya pekee ya kuwafikishia mizigo yao kwa muda mfupi na kwa usalama zaidi, ikiwepo sababu za kiutendaji.

iii. Ujenzi wa 'Standard Gauge' uende sambamba na kuimarisha mawasiliano katika kuendesha shughuli za reli ili kuongeza ufanisi.

iv. Ili kufupisha muda wa ujenzi, kuwepo na wakandarasi ambao watapewa vipande vidogo vya takribani kilomita 200 ambavyo vitajengwa kwa

wakati mmoja ili kuwezesha reli hii ikamilike kwa haraka.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa majibu niwapi , fungu lipi imetengwa bajeti ya kujenga reli ya umbali wa km 1,220 kutoka Tabora-kigoma, Isaka – Mwanza, Uvinza- Msongati na kaliua-Mpanda- Karema, reli ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano awamu ya Pili inapaswa kuwa imetengewa shilingi Billion 102.89.

### a. KUSHINDWA KUJENGWA KWA RELI NYINGINE

**Mheshimiwa spika**, Ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara-Mbambabay na matawi ya kwenda Liganga na Mchuchuma yenye umbali wa 1,000 km kwa kiwango cha standard gauge (bil 340.50), ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha-Musoma na matawi kwenda Minjingu na Engaruka (shilingi bilioni 110.43), ununuzi wa mabehewa ya mizigo 2,234 (shilingi bilioni 0.19) pamoja na ununuzi wa vichwa vya treni 63 (shilingi bilioni 0.26 ) ni miongoni mwa vipaumbele vya taifa hili ambavyo tulikubaliana katika mpango wa miaka mitano lakini ujenzi huu pamoja na ununuzi huu wa mabehewa hazionekani katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa spika**, Miradi ya maendeleo kwenye sekta ya Uchukuzi inaonesha kwamba serikali imetenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia za reli kwa standard gauge kati ya mtwara – Mbambabayi na matawi ya mchuchuma na Liganga;

Tanga- Arusha –Musoma pamoja na matawi yake kwenda Engaruka na Minjingu na njia mpya za reli katika jiji la Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Taifa linakuwa na mpango wa Maendeleo kama dira inayoliongoza Taifa, na kwa kuwa kuna shida ya kukosekana kwa kushabihiana kati ya Mpango wa Taifa wa miaka mitano na Bajeti ya Serikali kwa Wizara hii ni ishara tosha kwamba, serikali hii inaendeshwa bila kuzingatia vipaumbele vya taifa, kwa maana nyingine Bunge lako tukufu mheshimiwa spika linatumika kujadili na kuidhinisha mipango ambayo haiwezi kutekelezeka.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa niaba ya watanzania inataka kufahamu, ikiwa mpango wa taifa wa miaka mitano uliowasilishwa mbele ya bunge lako tukufu na kujadiliwa bungeni uliandaliwa na Serikali hii ya chama cha mapinduzi, na vipaumbele vya kutekelezwa viliidhinishwa na Serikali hiyo hiyo na kwa kuwa pia bajeti za serikali inaandaliwa na serikali hiyo hiyo lakini vitu hivi viwili vinakuwa tofauti. Hii ni ishara kwamba serikali hii haina mipango wala mikakati mbadala ya kushughulikia matatizo ya watanzania na matokeo yake mpango huu utashindwa kutekelezwa kama ambavyo mipango iliyotangulia ilishindwa.

**Mheshimiwa Spika,** maendeleo hayawezi kupatikana bila ya kuwa na nidhamu ya kutekeleza mipango tuliyojiwekea

wenyewe na nidhamu inayoongelewa ni kuwa na bajeti ya utekelezaji wake.

## VIII. RELI YA TANZANIA NA ZAMBIA (TAZARA)

**Mheshimiwa Spika**, Reli ya Tazara iliyojengwa miaka ya 1970 ikitokea Dar es Salaam hadi New Kapirimposhi Zambia, uwezo wake wa kusafirisha mizigo na abiria umeshuka sana kutokana na sababu mbalimbali. Aidha Reli hiyo yenye uwezo wa kubeba tani milioni tano za shehena kwa mwaka, hivi sasa inaweza kubeba tani 100,000 tu kwa mwaka, sababu kubwa ni uchakavu wa miundombinu kama vile njia ya reli, injini na mabehewa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na matatizo yanayoikabili TAZARA ili iweze kujiendesha kibiashara lakini inaonekana serikali pamoja na menejiment ya TAZARA kwa pamoja wako "busy" wakifanya siasa badala ya kufikilia namna bora ya kulifanya shirika hili kujiendesha kwa faida.

**Mheshimiwa spika** changamoto zinazoendelea kulikwamisha shirika la reli la TAZARA zinatokana na ufdhaili, umiliki wake pamoja na sheria inayoisimamia. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na;

i. uchakavu wa miundombinu, kama injini na mabehewa ambayo yamepitwa na wakati kwa kipindi kirefu sasa na TAZARA kushindwa kujiendesha kwa faida kwa kipindi kirefu,

ii. TAZARA kushindwa kulipa mishahara kwa wafanyakazi wake na kutegemea serikali kuwalipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara na huku likiendelea kufanya biashara kwa hasara.
iii. Changamoto zinazotokana na mapungufu ya sheria namba 23, ya mwaka 1975 kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria namba 4 ya mwaka 1995.
iv. Wanahisa kutegeana na kutoa kipaumbele kwa reli zinazomilikiwa na kwa 100% na nchi husika kwa mfano TRL, RAHCO na NRZ.
v. Deni kubwa linalofikia Trilioni moja.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli uliodhahiri kwamba TAZARA haitaweza kujiendesha kwa faida kama mabadiliko makubwa ya kiutawala hayatafanyika. Pamoja na mapendekezo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni 2016/17 iliyatoa katika hotuba yake, inaonekana kama mawazo hayo hayakupewa kipaumbele kwa kiwango cha kutosha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa majibu ya mambo yafuatayo:

**Kwanza,** Ni lini serikali itaweka mikakati thabiti ya kuiwezesha TAZARA kujiendesha kwa faida kuliko ilivyo sasa?

**Pili**, serikali itaendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA hadi lini na ni mkakati gani ambao serikali ilifanya na au inafanya ili kumaliza matatizo ya menejimenti ambayo yamekuwa yakijitokeza, ikizingatiwa kwamba

viongozi waliopo wanadaiwa kutozingatia utawala bora, uwazi na uwajibikaji?
**Tatu,** Kwa kuwa matataizo yaliyo mengi inaonekana kuwa ni matokeo ya madhaifu ya kisheria yaliyoko kwenye sheria namba 23 ya mwaka 1975, kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria namba 4 ya mwaka 1995, je Serikali inampango gani wa kuleta bungeni marekebisho ya sheria hiyo ili kuondoa changamoto hiyo inayokwamisha TAZARA kusonga mbele.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM imekuwepo madarakani kwa kipindi chote cha uhai wa reli hii kamwe haitakwepa lawama na dhambi kubwa ya reli hii kutoweka.

**Mheshimiwa Spika,** yaliyotokea na yanayoendelea kutokea TAZARA yatoe funzo na iwe darasa kwa nchi yetu katika kuendeleza na kusimamia reli zetu. Hivi sasa nchi inajenga reli ya kati kwa kiwango cha standarg gauge kwa takribani kiasi cha shilingi Trilioni 17 wakati TAZARA ilijengwa kwa kipindi hicho  dola milioni mia mbili hamsini.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka seriakali kuweka mpango mahususi wa kuifanyia marekebisho reli hiyo na hivyo tunaona kwamba mapendekezo ya kambi yakifanyiwa kazi TAZARA inaweza kusimama imara na ikajiendesha kwa faida.

**Mheshimiwa Spika**, mfuko wa maendeleo ya reli ambao tulishauri uundwe na ukaundwa siku za hivi karibuni umetumika bayana kuwa utatumika kwa miradi ya miundombinu ya reli nchini na tunauhakika kwamba kama

matumizi ndiyo yale yaliyopelekea uanzishwaji wake basi matawi mengine ya Reli yatajengwa kwa kiwango cha standard gauge bila ya uhitaji wa kukopa fedha kwa masharti ya kibiashara kama ambavyo inafanyika hivi sasa.

## F. SEKTA YA MAWASILIANO

### a. ANUANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Anuani za makazi na Postikodi ulizinduliwa Sept 2016, hapa Dodoma unatekelezwa kwa kasi ndogo sana na ni wananchi wachache wanaoufahamu mpango huu.

Mpango huu unaumuhimu mkubwa katika kuwezesha ufikishaji wa huduma mbalimbali kwa haraka kwa jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa watanzania ili wapate uelewa mpana kuhusu mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utekelezaji wa mradi wa majaribio katika baadhi ya maeneo katika mikoa ya Dodoma, Arusha, na Dar es Salaam, sasa mpango uliopo ni Serikali za mitaa kuendeleza katika maeneo yao. Kambi Rasmi ya Upinzani inao wasiwasi mkubwa kama kweli Halmashauri zitafaulu kutokana na kuwa na fedha kidogo wanazokusanya kuweza kukidhi mpango huu. Kwa sababu hiyo tunaitaka Serikali (TAMISEMI) itenge bajeti maalum ya kuendeleza mpango huu muhimu katika kufikisha huduma kwa haraka, kinyume na hapo hata uwekezaji uliokwisha fanyika utakuwa ni kazi bure.

## b. SHERIA YA MAKOSA YA MTANDAO NAMBA 14 YA MWAKA 2015

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kwamba Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, akitoa maoni ya kambi mwaka wa fedha 2016/2017 alilieleza bunge lako tukufu jinsi ambavyo Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha sheria namba 14 ya mwaka 2015 tarehe 1.4.2015. Pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupinga kupitishwa kwa sheria hiyo kutokana na kuwepo kwa vifungu ambavyo vilikuwa vinaminya uhuru wa utoaji na upokeaji wa taarifa kwa njia ya mtandao na baadhi ya wabunge wake wakiwasilisha majedwali ya marekebisho kwa ajili ya kufuta au kurekebisha vifungu kandamizi, lakini sheria hiyo ilipitishwa na bunge lako tukufu kutokana na wingi wa wabunge wa CCM kwa kuwa walipinga marekebisho hayo.

**Mheshimiwa Spika,** zipo kila dalili zinazoonesha kuwa Sheria hiyo kandamizi ilitungwa kwa mashinikizo ya Chama tawala kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 kutokana na kasi ya vijana ambao wengi ndio watumiaji wa mitandao ya kijamii nchini ambao wengi walikuwa wakiunga mkono upinzani. Mara baada ya kumalizika uchaguzi mkuu, ushahidi unaonesha kuwa Sheria hii mbaya ilitungwa kwa makusudi ya kuwabana watanzania ambao wapo tayari kukosoa utendaji mbovu wa awamu ya tano na kuleta utawala wa kiimla na kidikteta katika taifa hili changa ambalo mpaka sasa halijafanikiwa kuwa taifa la uchumi wa kati.

**Mheshimiwa Spika,** Taifa limeathirika kwa namna moja au nyingine kwa kitendo cha MCC kuiondoa Tanzania kama mnufaika wa misaada yake kutokana na tamko la uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya MCC iliyotolewa tarehe 28 Machi 2016 kuwa mojawapo ya sababu za Tanzania kuondolewa katika MCC ni uwepo wa Sheria ya Makosa ya Mitanado ambayo imetumika kama mojawapo ya njia za kuminya uhuru wa mawazo, ikiwemo kukamatwa kwa baadhi ya watu kwa makosa yanayohusiana na mitandao kipindi cha uchaguzi. Zaidi, tamko hilo lilieleza kuwa mazingaombwe na marudio ya uchaguzi wa Zanzibar tarehe 20 Machi 2016 na Sheria kandamizi ya Makosa ya Mitandao vinakinzana na azma ya uwepo wa demokrasia na uchaguzi huru na wa haki. Hivyo MCC ikatangaza kuvunja utekelezaji wa mpango wa pili wa maendeleo wa MCC kwa kushirikiana na Tanzania. Mojawapo wa sekta zilizokua zikipokea fedha za MCC ni sekta ya ujenzi wa miundombinu. Baadhi ya miradi iliyokuwa inafadhiliwa na MCC kwa Sekta ya Ujenzi nchini Tanzania ni pamoja na; Mradi wa Barabara, kilometa 67 kutoka Songea-Namtumbo, Mtwara corridor, Tanga – Horohoro, Tunduma na Mafia Island airport.

**Mheshimiwa spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua hatua ya miradi hiyo iliyokuwa ikifadhiriliwa na MCC, pamoja na ukweli mchungu uliojificha kwamba huenda miongoni mwa sababu za kwanini serikali imeshindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo hata

kwa nusu ya bajeti ni matatizo kama haya ya kusitishwa kwa miradi ya ufadhiri.

## G. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuhitimisha kwa kusema kuwa Kushindwa kutekelezwa kwa bajeti kwa kiwango kinachoridhisha ni matokeo ya matendo ya serikali na kushindwa kutekeleza miradi ambayo imepangwa kutekelezwa na Serikali yenyewe. Huu ni udhaifu mkubwa, kama mpangaji wa mipango ni wewe na wewe ndiye unashindwa kutoa fedha za utekelezaji, je ni nani anatakiwa kutekeleza mipango hiyo? Hoja kuwa ni masuala yasiyokuwa kwenye mipango kupewa nafasi kubwa kuliko mipango iliyopangwa na kupitishwa na Bunge. Kwa maneno mengine hii ni dharau kwa Mhimili huu unaoisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mpango wa miaka mitano 2016/17 – 2020/21 **"Nurturing Indusrialization for Economic Transformation and Humana Development"** ni mpango uliopitishwa na Bunge hili na kwa vyovyote vile ndio dira ya mipango mingine yote inayoletwa ili kupata idhini ya Bunge letu. Hivyo basi kutokuzingatia mipango ambayo tayari ilikwishapata Baraka za Bunge na kuleta mambo mengine inatufanya tutafakari kwamba, mpango huo ulikuwa ni wa njonzi za mchana na baada ya Serikali kuona kwamba hautekelezeki inaanza kuukimbia kwa kuleta mipango mingine. Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kwamba mpango bila fedha za utekelezaji ni bure na ni hadaa tupu.

Kwa maana hiyo, tunaomba tufahamishwe je, Bunge ndilo lililopigwa changa la macho kwa kupitisha mpango hewa? Au Serikali ndiyo inashindwa kuwa makini katika utoaji fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo? Huo uchumi wa viwanda tutaufikiaje kwa kutokuzingatia yale tuliyokubaliana?

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

……………………………………………………..

**WILLY Q.QAMBALO (MB)**

k.n.y Waziri Kivuli wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

**27 April 2017**